

TANGAZO LA ZABUNI

TANGAZO LA ZABUNI YA UBLIA WA KUJENGA, KUENDESHA NA KUKABIDHI MRADI WA UJENZI WA UCHIMBAJI NA UCHAKATAJI WA KOKOTO NA MAWE KATIKA MGODI WA MADINI YA UJENZI ENEO LA MAZINGARA HANDENI

LGA-129/2023-2024/C/01

20/02/2024

1. Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ambaye ni mmiliki wa Mgodi wa Madini ya kokoto (madini ya ujenzi) uliopo katika Kijiji cha Mazingara, Kata ya Mazingara, inakusudia kutafuta mbia atakayejenga, kuchimba, kuendesha na kurejesha mradi wa uchimbaji madini hayo.
2. Halmashauri inakaribisha maombi ya zabuni ya ubia wa kuendeleza Mgodi huu kwa kujenga miundombinu ya kiwanda cha uchakataji kokoto na mawe, kuendesha shughuli za uzalishaji wa kokoto na mawe ya ujenzi na baadae kurejesha kwa mmiliki wa Mgodi. Mbia atatakiwa kuendesha Mgodi kwa kuleta mitambo ya kupasua na kusaga kokoto na mawe ya ujenzi kwa viwango tofauti.
3. Hivyo wazabuni mbalimbali wenye sifa, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hii kwa niaba ya Halmashauri wanaalikwa kuomba zabuni hii.
4. Wazabuni ambao wanania ya kuendeleza mgodi huu kufika na kukagua eneo la mradi pamoja na kukagua nyaraka za zabuni kwenye Ofisi ya Manunuzi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 siku za kazi Jumatatu hadi Ijumaa.

MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awasilishe andiko la mradi (business proposal) pamoja na mambo mengine aoonyeshe takwimu za uzalishaji wa kokoto na mawe ya ujenzi kwa mwaka
2. Waomabi wenye Kampuni waambatanishe nyaraka zote muhimu za Kampuni
3. Mwombaji atoe udhibitisha wa uwezo wa kifedha (financial capacity) alionao ili kuthhibitisha uwezo wa kutekeleza shughuli za mradi
4. Mwombaji aonyeshe aina ya mitambo ya uzalishaji atakayotumia kwenye uzalisha katika kipindi cha mkataba na aainishe uwezo wa uzalishaji wa mitambo hiyo
5. Mwombaji aonyeshe kiwango atakachoilipa Halmashauri kutokana na uzalishaji na uuzaaji wa kokoto na mawe


6. Mwombaji atatakiwa kutaja majina ya Wakurugenzi/Mkurugenzi wa Kampuni na kutaja mahali Ofisi ya Kampuni ilipo na aambatanishe na wasifu wa Kampuni yake (Company Profile)
7. Mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kulipa ushuru na kodi zote za serikali kwa mujibu wa sheria
8. Mzabuni atatumia mashine za kieletroniki za Serikali kutoa stakabadhi kwa mauzo yote ya bidhaa iliyozalishwa kwenye mgodi na kuuzwa
9. Mwombaji aonyehe uzoefu wa shughuli za uendeshaji crasher
10. Mkataba utatolewa kwa mwombaji atakaye shinda zabuni
11. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa kuleta barua ya maombi na malipo ya fedha taslimu yasiyorudishwa (nonrefundable) ya fedha za kitanzania shilingi **laki moja tu (Tshs. 100,000)** kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni S.L.P 355 Handeni
12. Zabuni zote ziwasilishwe kwenye sanduku la zabuni lililopo katika ofisi za mapokezi za Halmashauri ya Wilaya ya Handeni au zitumwe kwa kifurushi maalum (registered mail) ili zifike kwa wakati kabla ya tarehe ya mwisho ya uwasilishaji (deadline). Waombaji watume zabuni kwa:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P 355
Handeni**

Zabuni zifungwe kwenye bahasha mbili na bahasha ya nje iandikwe Zabuni Namba na Jina la Zabuni na iwekwe lakiri

13. Mwisho wa kupokea zabuni ni siku ya Alhamisi tarehe 5/03/2024. Saa 6.00 mchana. Mara baada ya hapo zabuni zitafunguliwa kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri hivyo waombaji au wawakilishi wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi.

14. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni za kielectroniki na ambazo hazikupokelewa, na hazikufunguliwa na hazikusomwa mbele ya hadhara kwenye sherehe ya ufunguzi hazitakubaliwa kufanyiwa tathmini.



**SAITOTI Z. STEPHEN
MKURUGENZI MTENDAJI
H/W HANDENI**